# LEARNING BY EAR

## Lent Luxury-The risks of raising credit

## EPISODE FIVE: THE SECURITY RISK

**AUTHOR: James Muhando**

**EDITORS: Adrian Kriesch, Friederike Müller**

**PROOFREADER: Tony Dunham**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**LIST OF CHARACTERS - EPISODE FIVE.**

**SCENE ONE: AT THE POLICE STATION.**

- **LUKA(M 40’S)**
- **JD(M 15)**
- **POLICEWOMAN (F 35)**
- **OFFICER (M 50)**
- **NARRATOR (M 30)**

**SCENE TWO: GORI STRIKES.**

- **NARRATOR (M 30)**

- **GORI (M 45)**
- **JENNY (F 15)**
- **GIDDY (M 15)**
- **TWO MEN (ADULTS)**

**<u>SCENE THREE: AT THE MARKET PLACE.</u>**

- **4 SELLER (F/M age not important)**
- **ZILPAH (F 35)**
- **EUNICE (F 35)**
- **NARRATOR (M 30)**

**<u>SCENE FOUR: AT THE HOSPITAL.</u>**

- **GIDDY (M 15)**
- **JENNY (F 15)**
- **NARRATOR (M 30)**

**<u>SCENE FIVE: WHO ARE THESE MEN?</u>**

- **NARRATOR (M 30)**
- **THUG 1 (M 40’S)**
- **THUG 2 (M 40’S)**
- **GIDDY (M 15)**

**<u>INTRO:</u>**

**1. SFX: AMBIENCE NEXT TO SWIMMING POOL**

**2. Narration:** Hujambo na karibu katika sehemu ya tano ya mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo jenga Maisha yako. Tukiwa bado katika ile hadithi kuhusu “Sterehe ya Kuazima- Tatizo la kulipa Mkopo” *.* Niko katika kidimbwi cha kuogelea! Bado wanikumba? Mimi ni Gideon Leboo afisa wa masuala ya mikopo kwenye benki hii ya Jubilee. Najua tayari unafikiria nini: Pengine huyu mtu ni mtu tajiri akijivinjari katika kidimbwi cha kuogelea (laughs). Lakini umekosea! Mara nyingi nakasirika sana watu wakiniita Tumbo tumbo, kama rafiki yangu Jenny alivyokuwa akiniita shuleni! Hii ndio sababu nataka kupunguza mwili. Lakini kusema kweli siwezi kuogelea kwa muda mrefu. Nikitumbukia kwa maji dakika moja tu, natoka nje kujianika kwa jua **(Laughs).** Kwa hivyo badala ya kujianika hapa, hebu turudi nyuma kidogo katika hadithi yetu, wakati nilipokuwa shuleni. Kila mmoja alinifahamu kama Giddy.Katika kipindi kilichotangulia, tulisikia mjomba Barry akiomba mkopo kutoka kwa Bw. Mando baada ya kuzongwa na madeni. Haya ndio makosa tuliyofanya wakati tulipokwenda kuchukua mkopo kutoka kwa Gori. JD alikuwa amechukua baiskeli kwa mkopo baada ya kughushi sahihi ya babake ili kupata mkopo huo uliomweka mashakani. Wakati babake alipofahamu ukora huo, alikwenda moja kwa moja hadi shuleni na

kumvuta masikio JD kumtoa darasani. JD alikuwa na wasiwasi maana hakujua babake anampeleka wapi.

**SCENE ONE: AT THE POLICE STATION.**

3. **DOOR OPENS, FOOTSTEPS AS DAD DRAGS SON**
4. **LUKA:** Twende, wewe kijana mjinga sana!
5. **JD:** **(Crying and sobbing)** Tafadhali baba usinipeleke polisi. Baba nisamehe!
6. **LUKA:** Lazima utakiona cha mtema kuni! Sikujua kwamba nalea mhalifu!
7. **JD:** Lakini watanifunga baba!
8. **LUKA:** Ulipaswa kulifikiria hilo kwanza kabla ya kufanya uovu huo ulioyofanya!
9. **LUKA:** Keti hapa kwenye ubao! Na usijaribu kutoroka! Maafisa wa polisi watakukamata ukijaribu kufanya hivyo... **(Shouts to the officer)** Tafahali maofisa nichungieni huyu kijana!
10. **POLICEWOMAN: (From a distance)** Hakuna shida!
11. **SFX: FOOTSTEPS, KNOCK ON DOOR.**
12. **OFFICER:** **(From inside)** Pita ndani.
13. **SFX: DOOR OPEN. FOOTSTEPS. DOOR CLOSE**
14. **LUKA:** Habari Ofisa!

**15. OFFICER:** Oh, Ni wewe tena, Luka! Umemleta kijana?

**16. LUKA:** Kama tulivyozungumza mapema!.Hebu mfunzeni adabu kidogo huyu kijana wangu. Lakini tafadhali msimfungie kwenye seli ya kawaida ya wahalifu sugu. Nataka tu mumfunze adabu.

**17. OFFICER:** Usijali Luka! , Yuko mikononi mwa maafisa wa usalama, njoo umchukue kesho asubuhi.

**18. NARRATOR:**

Na hivyo ndivyo rafiki yangu alivyoishia mikononi mwa maafisa wa usalama! Lakini si mkono wa sheria pekee uliotukosesha usingizi, bali pia deni la Gori ambalo bado tulikuwa hatujalilipa, kutokana na ukosefu wa pesa! Nyumbani katika kijiji nilikozaliwa, wakati wa likizo ya mwezi Desemba, mara kwa mara tuliweza kupata pesa wakati wa mavuno ambapo vibarua huwa na vingi! Kwa hakika tungeweza kuulia mkono wa Gori. Riba ya mkopo huo tayari ilikuwa imeanza kuwa kubwa baada ya kukosa kulipa kwa muda mrefu. Hivyo tuliamua kubadilisha njia yetu ya kawaida kwenda shule ili kumtoroka Gori. Lakini Gori hakuwa mjinga, na si bure akaitwa Papa . Alituandama na kutushika tukiwa njiani kwenda.

**<u>SCENE TWO: GORI STRIKES</u>**

**19. SFX: COUNTRY SIDE ROAD, LITTLE TRAFFIC.**

***KW begin***

**20. JENNY:** Twende tukamtembelee JD.

**21. GIDDY:** Kwani ameachiliwa na polisi?

**22. JENNY:** Tobby anasema hivyo!

**23. GIDDY:** Amejuaje?

**24. JENNY:** Wewe tumbo tumbo! Babake Tobby anafanya kazi katika kituo hicho cha polisi,.. kwani umesahau?.

**25. GIDDY:** **(Remembers)** Ahhh, ni kweli hata nilikuwa nimesahau (**Pause)**

***KW end***

**26. JENNY:** **(Scared)** Giddy, upesi basi!

**27. GIDDY:** **(Not worried)** Jenny! Unafikiri utanitisha?

**28. JENNY:** Huyo nyuma yako! Ni Gori!

**29. GIDDY:** **(annoyed)** Wacha mchezo!

**30. JENNY:** Toroka! Giddy! Toroka!

**31. SFX: FOOTSTEPS AS SHE STARTS TO RUN**

**32. GORI:** **(Aggressive)** Kujeni hapa nyinyi watoto wajinga! Wapi pesa zangu!

**33. SFX: RUNNING FOOTSTEPS (Jenny, Giddy and Gori)**

**34. GIDDY:** **(Screams and runs)**

**35. SFX:** **SOMEONE STUMBLES AND FALLS. (Jenny's and Gori's footsteps stop**

**36. SFX:** **FOOTSTEPS (Giddy) continue as he keeps running away**

**37. JENNY:** **(In pain)** Ah, mkono wangu! umevunjika!

**38. GORI:** **(Catches her)** Njoo hapa wewe! Unafikiri unaweza kumtoroka Gori? Unadhani unaweza kuchukua pesa zangu kisha utoroke?

**39. JENNY:** **(Calls out)** Giddy, Nisaidie! Usiniache peke yangu hapa!

**40. GIDDY:** **(From a distance)** Mwache rafiki yangu!

**41. GORI:** Unafikiri unaweza kunitapeli? Kuja hapa !

**42. JENNY:** **(In pain)** Mkono wangu, uuuuui! Waniumiza!

**43. MAN1:** Wewe..!, Kunaendelea nini hapa?

**44. GORI:** **(Chuckles in pretence)** Ni huyu msichana! Nadhani ameanguka na kuvunja mkono wake. Hawa watoto ni watukutu sana? **(Whispers menacingly to Jenny)** Ukijaribu kusema chochote nitakuua. Unasikia ?

**45. SFX:** **VEHICLE APPROACHING.**

**46. MAN2:** Simamisha hilo gari. Haraka tumpeleke hospitalini!

**47. SFX:** **VEHICLE STOPS.**

**48. MAN 1:** Haya ...tumbebe !

**49. MAN2:** Taratibu. Usije ukamuumiza zaidi mkono wake!

**50. MAN 1 + 2:** **THEY LIFT HER.**

**51. MAN1:** Huyu mtu ametorokea wapi?

**52. MAN2:** Na si huyu ni Gori? Yule mwenye kukopesha pesa?

**53. SFX:** **RUNNING FOOTSTEPS APPROACHING.**

**54. GIDDY:** **(Arrives panting)** Ni Gori! Alikuwa akitufukuza ndio Jenny akaanguka na kuvunjika mkono!

**55. MAN1:** Akimfukuza? Kwanini?

**56. JENNY:** **(Crying)**

**57. GIDDY:** Rafiki yetu mmoja alimkopa pesa na hatujamlipa.

**58. MAN2:** Mmekopa pesa za Gori? Kwani nini nyinyi watoto?

**59. MAN1:** Hebu twende tukamtafute Gori!

**60. MAN2:** Wewe nenda. Mimi lazima kwanza nimpeleke huyu msichana hospitalini. Twende dereva!

**61. SFX:** **VEHICLE STARTS, CAR DOOR CLOSES, DRIVES OFF**

**62. NARRATOR:**

Hatukuweza kumkamata Gori ambaye alifunga duka lake kwa muda mrefu. Kisha ikatokea kwamba mamake Jenny alikwenda kuripoti kisa kicho kwa polisi, ambao mara moja walianzisha msako wa kumtafuta Gori. Mkopo huo sio tu umemtia mashakani JD bali pia sisi rafiki zake

wasio na hatia. Yaani kukopa ili kulipa mkopo mwengine si suluhisho bali ni njia ya kujilimbikizia matatizo, na ambapo ni hatari zaidi! Katika kisa hiki, hata mamangu Zilpah na rafiki yake Eunice pia walihusishwa! Hebu tusikilize kilichowapata baada ya Mimi na Jenny kumtoroka Gori.…

**SCENE THREE: AT THE MARKET PLACE.**

63. **ATMO:** **MARKET PLACE AMBIENCE, SEVERAL SELLERS SHOUTING.**

64. **SELLER 1 :** Nguo za mitindo ya kisasa! Tunauza nguo!

65. **SELLER 2:** Tomato, *freshi* kabisa kutoka shambani..Tomato..,!

***KW begin***

66. **EUNICE:** Kilo moja ya tomato tafadhali!

67. **SELLER 2:** Hizi hapa Mama ....! kilo moja ni dola moja!

68. **EUNICE:** Shika pesa zako!

69. **SFX: COINS JINGLE.**

70. **SELLER 2:** Asante sana Mama! **(Shouts)** Tomato *fershi* kabisa kutoka shambani! Tomato *freshi* kutoka shambani! !

***KW end***

71. **EUNICE:** Zilpah, Nilifikiri unataka kununua Tomato.

72. **ZILPAH:** **(Silence)**

**73. EUNICE:** Zilpah? Zilpah! Unaota nini!

**74. ZILPAH:** **(Comes back)** Uhhh! ndio! Eunice! Umesema nini?

**75. EUNICE:** Akili yako iko mbali sana? Una tatizo gani?

**76. ZILPAH:** Hata sijielewi naona nashikwa na wazimu, lakini naona hawa wanaume wawili wanatufuata!

***KW begin***

**77. EUNICE:** Wanaume gani?

**78. ZILPAH:** Hawa wako nyuma yangu, mmoja amevalia kofia ya rangi ya samawati na mwengine amevalia jezi ya hudhurungi! Nimewaona wakitufuata tangu tukitoka nyumbani.

***KW end***

**79. EUNICE:** **(Dismissive)** Wewe unaota !Kwanini watufuate?

**80. ZILPAH:** Katika muda wa hivi punde nimekuwa nikijihisi hivyo sijui kwanini. Naona kana kwamba kuna mtu ananichunguza .

**81. EUNICE:** Nunua kile unachotaka kununua twende! Tunachelewa!

**82. NARRATOR:**

Labda Eunice angemsikiliza Mamake! Ni kweli kuna watu wawili wanaowafuata. Na walipokuwa wakienda nyumbani, Mamake Eunice anagundua kwamba, kweli kuna watu wawili ambao wamekuwa

wakiwafuata nyuma! Watu hawa wawili ni kina nani na watanaka nini? Kwa upande mwengine, Jenny amepata fahamu na kujikuta na bandeji mkononi akiwa katika kitanda cha hospitalini.

**SCENE FOUR: AT THE HOSPITAL.**

**83. GIDDY:** Unajisikiaje sasa?

**84. JENNY:** **(Unhappy)** Nasikia maumivu sana!

**85. GIDDY:** Pole sana Jenny!

**86. JENNY:** **SILENT.**

**87. GIDDY:** Pole sana ningekuwa nimekusaidia, lakini Gori alinitisha na nikatoroka!

**88. JENNY:** Uliniacha peke yangu na yule jambazi!

**89. GIDDY:** Lakini ningefanya nini Jenny?

**90. JENNY:** Ungekabiliana naye kama mwanamume, ukapiga kelele ili kutafuta usaidizi!

**91. GIDDY:** Sasa unanilaumu?

**92. JENNY:** Ndio nakulaumu Giddy! Nilikwambia Gori ni mtu hatari sana lakini hukunisikiliza! Ulisema marafiki huwa wako tayari kufa pamoja , au sivyo? Na kwanini ukaniacha peke yangu wakati nimepatwa na shida, nikihangaishwa na Gori?

**93. GIDDY:** Sijui niseme nini Jenny! Samahani!

**94. JENNY:** Ondoka!

**95. GIDDY:** Jenny, tafadhali!

**96. JENNY:** Ondoka nende zako!

**97. SFX: FOOTSTEPS AS GIDDY LEAVES**

**98. NARRATOR:** Hebu fikiria nilisikiaje nilipokuwa nikiondoka. Jenny ni rafiki yangu mkubwa sana! Na sasa ananilaumu kwa yote yaliyotokea? Lakini nilimlaumu sana JD! Nilipokuwa nikienda nyumbani, nilikuwa nikiwaza na kutumai kwamba mamangu hajapata habari kuhusu yaliyotokea. Nilitembea pole pole kupitia bustani yetu iliyojaa miti, huku giza likiwa limeanza kuingia. Nilisikia wanaume wawili wakizungumza kwa sauti za chini sana. Je walikuwa wakifanya nini katika bustani yetu usiku huo? Walikuwa hawajaniona!

**<u>SCENE FIVE: AT GIDDY'S.</u>**

**99. SFX: NIGHT SOUNDS IN THE VILLAGE, OUTSIDE**

**100. THUG 1:** Una hakika ni hapa ?

**101. THUG 2:** Lakini si ulimuona akitembea kuja huku, ama sivyo?

**102. THUG 1:** Lakini sikumanisha anaishi hapa!

**103. THUG 2:** Kunauwekana kwamba haishi hapa.lakini amekuja kujificha

**104. THUG 1:** Sasa tufanyeje?

**105. THUG 2:** Tusubiri hadi atakapotoka nje.

**106. THUG 1:** Na hii baridi yote? Twende nyumbani tutarudi kesho.

**107. THUG 2:** Na mkubwa wetu atasema nini endapo atatoka hapa na kutoroka kwenda kujificha sehemu nyingine? Tumeagizwa tusiondoke hapa hadi tumpate.

**108. THUG 1:** Pengine wale wanawake wawili waliokuwa wakitoka sokoni wametuona.

**109. THUG 2:** Hizo ni dhana zako, tusubiri hapa tu pengine anaweza kutoka nje na atoroke!

**OUTRO:**

**110. SFX: SWIMMING POOL ATMO**

**111. NARRATOR:**

Na kwa hadithi hiyo kuhusu ujana wangu ndipo tunafika mwisho wa kipind cha leo. Ungana nasi tena katika kipindi kitakachofuata ili kusikia wahalifu hao wawili walikuwa kina nani na walikuwa wakitafuta nini! Pia tutasikia iwapo tulifanikiwa kusuluhisha matatizo yetu. Endapo ungepenza kusikiliza tena kipindi hiki, tembelea mtandao wetu wa dw.de/lbe. Asante kwa kutusikiliza hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa. (laughs). (as he jumps in)!

**113. SFX: PERSON JUMPS IN WATER**